*Jiwe la kiroho la kujengea  No.87*

# KUITWA KULINGANA NA KUSUDIO LA MUNGU

**Warumi 8:28-30***,* *"Nasi twajua ya kua katika mambo yote Mungu  hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa* ***kwa kusudi lake****."*

Hebu tusikilize kile nabii wa Mungu anachosema kuhusu hilo:

Kama una Uzima wa Milele(Yohana5:24), kuna wa aina moja tu, huo ni Mungu, nawe ni sifa iliyodhihirishwa. Unaona? Kama wewe…Kama sivyo ulivyo, hutakuweko, hata hivyo. "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu." (Yohana6:44).

Roho Mtakatifu ni wa Milele. Halafu, wewe uko katika Umilele, mahali ulipokuwa wakati wote, lakini umetambua tu hivi punde jambo lililotukia. Unaona, wewe ulifanywa kwa ajili ya kusudi la Milele, kwa maana ulikuwa dhi-dhihirisho la sifa iliyokuwa ndani ya Mungu, ambaye alikuwazia na akakutamka; Naye akaifanya dunia apate kukutwaa toka kwake, na kukufanya mwanadamu. Ndipo dhambi ikaja ikapotosha njia Yake. Ulikuja, hata hivyo, bali ulikuwa umepotea pamoja na ulimwengu. Kwa hiyo Yeye akaja na kukukomboa, sifa iliyodhihirishwa, kisha anaikomboa dunia hii kwa njia ile ile. Halafu, kusudi Lake linaendelea. Mnaona? Loo! Haleluya! Loo! jambo hilo linanisaidia sana, kuwazia tu juu ya mambo yajayo.

Mungu, hapo mwanzo, wakati alipofikiria juu yako na kufikiria juu ya wengine namna hiyo, akajifikiria Mwenyewe kwamba anaweza kugusika. Hayo yalikuwa ni mawazo Yake. Mnaona? Kwa hiyo, Yeye aliyaonyesha mawazo Yake kwa Neno. Yeye alisema, "Hebu na iwe. Na iwe," na ikawa. [1]

Mungu huweka wakati na ana kusudi kwa ajili ya kila kitu afanyacho. Hakuna kitu kinachotukia kwa bahati mbaya tu kwa wale wampendao Bwana na wameitwa kulingana na wito Wake. Mnaona? Tumechaguliwa tangu zamani(Waefeso1:3-7). Na kila kitu hufanya kazi vizuri tu, kwa ajili ya jambo hilo, kwa kuwa Yeye hawezi kusema uongo. Naye alisema hiyo ilikuwa ndivyo, ya kwamba kila kitu kina wakati wake, majira yake, na kina njia yake. Na Mungu yuko nyuma ya kila msogeo. Na wakati mwingine unafikiri kwamba kila kitu kinaenda mrama. Ni juu yetu. Mambo hayo yanawekwa juu yetu, majaribu na fadhaa. Ni kujaribiwa, kuona vile tutakavyotenda kwa tukio Fulani.[2]

Kwamaana,hufanya kila jambo kufanya kazi pamoja nao wampendao kwaajili ya kuwapatia mema(Warumi 8:28-30). [3]

Kila kitu kina kusudi fulani. Mmekusanyika hapa asubuhi hii kwa kusudi fulani. Ninakula kwa kusudi fulani, ninyi mnapika kwa kusudi fulani. Sasa Kila kitu ni kwa kusudi fulani. Kanisa hili limejengwa kwa kusudi fulani. Hakuna kitu kisicho na kusudi na sababu.

Hebu na tuchukue tone la kawaida la wino na tuliangalie. Ni kitu gani? Tone la wino. Lilitoka wapi? Hebu na tuseme ni wino mweusi. Sasa, wino huo upo kwa kusudi fulani. Unaweza kuandika msamaha wangu kutoka gerezani. Unaweza kuandika msamaha wangu kutoka kwenye jela la mauti. Hiyo ni kweli? Inaweza kuandika Yohana 3:16, na kuokoa nafsi yangu kwa kuamini Hilo. Sivyo? Ama, unaweza kutia sahihi hati yangu ya kuuawa. Mnaona? Unaweza kunihukumu Mahakamani. Una kusudi fulani. Hiyo ni kweli? Kila kitu kimefanywa kwa kusudio(Mithali 16:4). [4]

Unapotambua: Tunafanya nini hapa? Tulitoka wapi? Ama ni nini sababu yetu ya kuwa hapa? Hatukuwekwa hapa tu kibahati, tuliwekwa hapa kwa kusudi na hatuna budi kutumikia kusudi hilo. Lakini bado tumerudi katika msingi wa hiari ya kujiamulia ambapo tunaweza kutumikia Hilo ama kulikataa Hilo, kama vile tu Adamu alivyofanya pale mwanzo. [5] Lazima uwe na mapenzi binafsi ya kufanya mapenzi ya Mungu. [6]

Wakati fulani uliopita Nilisoma hadithi ya Mmoja wa marais wakuu sana nafikiri taifa hili liliyepata kuwa naye:Abraham Lincoln. Sio kwa sababu alitoka Kentucky, bali ni kwa sababu alikuwa ni mtu mashuhuri. Hakupata elimu, bali hata hivyo alikuwa na kitu moyoni mwake, kusudi fulani.

Nampenda mtu mwenye ono. Ninawapenda watu walio na jambo fulani wanalopigania, sio tu kukaa vivi hivi, “Vema, chochote kijacho kitakuwa ni sawa.” Loo, fanya hima ushike kazi! Wala Lincoln hakuiruhusu elimu yake imzuie; alikuwa na jambo fulani la kufanya. Nafikiri kila Mkristo anapaswa kuwa jinsi hiyo, tafuta kusudio lako na uende ukalitekeleze.

Kuwa na kusudi fulani maishani, jambo fulani utakalofanya. Mungu amekuweka hapa; fanya jambo fulani kulihusu, kila mfuasi wa kila kanisa. [7] Unakusudi Fulani – lengo Fulani la kulenga (Waefeso 2:10) [8]

Huenda usiwe kitu ila mke nyumbani. Vema, unasema, “Ndugu Branham, sijafaya kitu maishani mwangu. Mimi si mhubiri.” Vema, huenda ikawa Mungu alikuleta hapa upate kulea jamaa ya watoto, kutoka kwenye hiyo jamaa ya watoto huenda itatokea jamaa nyingine ya watoto ambamo atatoka mhubiri ambaye atawapeleka watu milioni kwa Kristo. Ilibidi uwepo hapa. Upo hapa kwa kusudi fulani. Ulijua jambo hilo? [9]

Sisi viumbe wasiostahili, tunaostahili jehanum, bali neema Yake inatushikilia kupitia hiyo. Angalia ni wangapi waliopotea na ni vipofu! Ni wangapi, ni wenye dhambi wangapi waliokuweko ulimwenguni, ile saa niliyookolewa! Mungu aliniokoa kwa kusudi fulani; nami nimeazimia, kwa mapenzi Yake, kutekeleza kusudi hilo. Sijali ni jambo lingine gani litakalotukia; nataka kulitekeleza.

Na katika saa ninapoona makanisa yote, madaha yao makuu, “na tajiri, na hatuna haja ya kitu,” wanasema; na kuwaona, wenye mashaka, wanyonge, vipofu(Ufunuo 3:15-19); halafu wanakupigapiga mabegani, wanakutaka upatane nao. Nilizaliwa kwa kusudi fulani, hilo ni kukilaani kitu hicho(Ulimwengu,mifumo ya kidini,mashirika,madhehebu); na kuwaita watoke. Nalitenda jambo hili. [10]

Sikilizeni! **Nataka** niwaambie kitu. Alikuwa na kusudi katika kuniokoa; alikuwa na kusudi katika kukuokoa(II Timotheo 1:9-10). Nami nimeamua, kwa mapenzi Yake, kulifanya, si kuliongeza au kulipunguza (Ufunuo 22:18-19), na kwa hiyo nimeamua kudumu na Injili kadiri niwapo hai kwa msaada wa Mungu.

Kumbuka! Hapa pana neema(warumi 3:23-26; waefeso 2:8-9). Kulikuwa na mamilioni wakifa katika dhambi aliponiokoa. Mimi nilikuwa nani kwamba angeniokoa? Alikuwa na kusudi katika kuniokoa, nami nimeamua kutekeleza kusudi hilo. Ninasukumwa kuelekea jambo hilo moja tu: Yesu Kristo na Umoja wa mwili wa Yesu Kristo.

Hilo ndio kusudio langu. Sijali; labda mwisho wangu waweza kuwa karibu sana sasa, lakini hata iwe nini, bado nimetia nanga. Sijaibadilisha kamwe.(Waebrania 6:8-20).

Mtu Fulani aliniambia akasema, “Billy, katika matatizo haya yote ulishikilia dini yako?”Nikasema, “La, bwana, ilinishikilia.” Unaona, unaona? Nanga yangu ilishikilia. Sikuishikilia kamwe, ilinishikilia. Siwezi kuishikilia; haiwezekani kamwe kufanya hivyo, lakini (Neema) inanishikilia. Ndio bwana.

Alikuwa na kusudi katika kuniokoa. Kulikuwa na mamilioni katika dhambi nilipomjia, lakini aliniokoa. Alikuwa na kusudi katika kufanya hivyo. Kifo cha Kristo kilikuwa Yakini kwa hofu yake.Kifo cha Kristo kilimaliza lile swala.(Waebrania 2:9-18). [11]

Mungu ni Mungu wa kweli(uhalisia). Usichukue tu kanuni. Usichukue tu msisimko. Chukua Uhalisia. Chukua Mungu wa kweli, jambo fulani Mungu alicho, Mungu wa kweli ambaye anakupa wewe Uhakika. Litakupa tumaini. Litakupa imani. Litakupa Roho. Litakupa ishara. Litakupa maajabu.Litafanya ndani yako kama lilivyofanya ndani ya Kristo. Kwasababu hilo ndio kusudio la kuja kwake: Kumleta Mungu ndani ya mtu, na kumfanya Mungu na mwanadamu kua mmoja.[12]

Nimekuwa Mmishenari, na kuona miungu mbalimbali na wanafalsafa; na hivyo ndivyo kila moja wa hizo ilivyo, nje ya Ukristo, ni falsafa tu, jinsi ambavyo wanaamini *hili, lile*, ama *linginelo*. Lakini yule Muumba mkuu aliyeumba viumbe! Hapana budi kuwepo na Muumba kama kuna uumbaji(wakolosai 1:16-17). Na kama kuna uumbaji, ulifanywa na Muumba(warumi 1:18-20). Na kazi ya mtu yeyote humwakisi mwenyewe. Yeye ni seremala mzuri, anafanya kazi nzuri, anajenga. Na endapo ni makanika mzuri, anafanya kazi nzuri. Kazi yako hukuakisi tu. Nao uumbaji wa Mungu humwakisi Mungu. Na Mungu aliumba kila kitu kwa kusudi fulani. Na kila kitu kinachotumikia kusudi la Mungu, wakati kinapokufa, kina ufufuo. Niambie kitu kimoja. Nami nilileta vitu vingi, kama maua na miti.

Na kama mtu anatumikia kusudi la Mungu, kuna ufufuo hakika kama chochote kile. Jambo pekee linalopaswa kufanya, ni, Mungu anangojea tu wakati, kama vile anavyofanya sasa.

Majani makubwa ndiyo kwanza yaanguke kutoka mitini, yameanguka, hasa. Ambapo mekundu, kijanikibichi, bluu, hudhurungi, rangi zote mbalimbali kote kwenye mapana ya nchi, ambapo viumbe vya Mungu vilikuwa chini yake vimekufa, Mungu alipanda tu shada lake la maua. Lakini Yeye anajua wakati anapopanda shada la maua, kuna ufufuo katika msimu wa kuchipua! Ulimwengu hauna budi kuja tu huku katika mzingo wake mpaka unaporudi moja kwa moja ukawa sawa na jua tena, nao utafufuka katika maua ya mazishi.(Ayubu 14:7-12)

Kamwe usiseme, “Huu ndio mwisho,” si zaidi ya vile majani, yaliyo na rangi ya hudhurungi mtini, yanavyosema huo ndio mwisho. Jambo pekee linalopaswa kufanya, ni duara la majira ya Mungu kuelea huku na huko, mpaka kwenye wakati wa kuja kwa Mwana wa Mungu. Na kila kiumbe kilicho hai kilichopata kufa katika Kristo kitafufuka tena. Katika Uwepo Wake, kumkumbuka Yeye. Loo, nitakapofikia mwisho wa safari yangu, ninataka kufa katika Uwepo Wake, nikimkumbuka, ya kwamba Yeye Ndiye ufufuo na Uzima(Yohana 11:25-26). Yeye Ndiye Huo. [13]

Kama kila kitu kinatumikia kusudi la Mungu, kina ufufuo. Bali kinaweza tu kufufuka kama kinatimiza kusudi la Mungu. Kama ua likiishi na halijarutubishwa, halitafufuka tena. Kama ukipanda mahindi, na hayajarutubishwa, hayatachipuka tena. Chochote kisichotumikia kusudi la Mungu, hakina ufufuo. Lakini huwezi kushikilia kitu chochote mavumbini kinachotumkia kusudi la Mungu. [14]

Huleta uhai wa mimea, kwa sababu Jua hutawala huo. Huwezi kuuficha. Hauna budi kuchipuka. Na yupo Mwana wa Mungu anayetawala uhai wa wanadamu, Uzima wa Milele. Na kama tunatumikia kusudi la Mungu, kama wana na binti za Mungu, na kurutubishwa kwa Roho Mtakatifu, kuzaliwa upya kwa Roho wa Mungu(yohana 3;3-8),basi wakati utakapokuwa tayari kwa Mwana wa Mungu kuja(ufufuo wa kwanza), usingeweza kuuficha Uhai huo wa Kiungu. Maumbile yote yanazungumzia Huo. [15]

Yesu alimleta Mungu katika maisha ya wanadamu. Mungu alifanyika mwanadamu. Wakati Yesu alipozaliwa, Mungu alifanyika mwanadamu, kwamba Yeye angefanyika ushirika na mwanadamu na ndani ya mwanadamu, ili atimize kusudio moja; hiyo ni, kuleta kwa wanadamu kile Mungu alicho; sio kile kile kanisa kilicho, lakini kile Mungu alicho. Yesu alikuja ili yeye aweze kumuwasilisha Mungu kwa wanadamu. Na mwanadamu hakulitaka hilo (yohana 1:1-18).

Na alipokuja,Waliamini kanuni za makanisa yao na mambo mpaka wakashindwa kuona uhalisia wa kile alichokijia; kumleta Mungu ndani ya mtu, kumfanya Mungu ndani ya mtu, kuwaunganisha wao pamoja tena. [12] Hilo ndio kusudio la Mungu kwetu sisi, kutuunganisha pamoja na kua mmoja. [16]

Sasa, kusudi la Mungu katika kumtuma Roho Mtakatifu lilikuwa nini? (Yohana 14:16-26). Kusudi la Mungu, tunaona hapa, katika kumtuma Roho Mtakatifu, lilikuwa kusudi moja, ya kwamba Mungu Mwenyewe apate kuishi katika Kanisa Lake na kuendeleza mipango Yake kupitia kwa Kanisa. Kwamba, Mungu alikuwa katika Kristo, akiendeleza mipango Yake kupitia kwa Kristo; kutoka kwa Kristo, kuingia Kanisani, kuendeleza kazi Yake kupitia kwa Kanisa. [17] Na sasa Mungu yuko ndani yetu. Yesu alisema katika Yohana 14:20 "*Siku hiyo mtajua kuwa Mimi niko ndani ya Baba, Baba ndani Yangu, Nami ndani yenu, nanyi ndani Yangu."* Mungu ndani yetu……Kusudi Lake lilikuwa nini? Kutekeleza mpango Wake.[18]

Basi hili hapa. Baba alikuwa Mungu juu yenu, tunasema. Tumekuwa tangu Adamu. Mungu, Baba, alikuwa juu ya Musa na wana wa Israeli, katika Nguzo ya Moto(kutoka 14:24). Halafu, Mungu pamoja nasi, katika Kristo(Isaya 7:14); akatembea pamoja nasi, akanena pamoja nasi, akala pamoja nasi, akalala pamoja nasi. Mungu juu yetu; Mungu pamoja nasi; na sasa Mungu ndani yetu. Yote aliyokuwa Mungu, yaliingizwa katika Kristo(II wakorintho 5:19); yote aliyokuwa Kristo, yaliingizwa katika Kanisa.Ni nini? Mungu akitenda kazi ndani yako. Po pote ulimwenguni ambapo angetaka kukuita, uko papo hapo, akifanya kazi pamoja nawe kutekeleza mapenzi Yake mema. Jinsi tunavyopaswa kumshukuru Mungu kwa sababu hiyo! Mungu, Roho Mtakatifu, anatumwa kwa kusudi la Mungu kuishi katika Kanisa Lake, akitenda kazi katika kila wakati, akitekeleza mapenzi Yake ya Kiungu.

*"Alikuja kwake, wala walio wake hawakumpokea. Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake*" (Yohana1:11-13). Loo ni jinsi gani tunapaswa kumpenda yeye na kumuabudu yeye! Kusudio la Mungu, alitaka kua katika ushirika…..[17]

Ushirika mkuu ambao mwanadamu angewahi kua nao ni ushirika na Kristo. Ninapenda kukutana na watu.Watu, wote tunapenda kua na ushirika mmoja kwa mwingine, wakati mwingine kutoka nje na kua na kitafunwa cha kula kidogo. Majirani wanawake wakizungumza kuvuka fensi, na kuja hapa na kua na sherehe kidogo walipokutana pamoja, ushirika.

Lakini ushirika Mkuu ambao kila mwanadamu angeweza kujua ni wakati anapokua katika Uwepo uliobarikiwa wa Mungu Mwenyenzi. Hakuna ushirika unaoweza kuchukua mahali pake.

Wakati mmoja mtu anapokua na ushirika mkamilifu na Mungu.Hilo ndio kusudio la Mungu. Hiyo ndiyo sababu ni tamanio ndani ya moyo wako, Ni shauku kwaajili ya jambo Fulani, mawasiliano. [19]

Mungu hufuata sheria Zake Mwenyewe. Ndipo, Mungu, kusudi alikomboe kanisa lililopotea, ulimwengu uliopotea, viumbe vyote vilivyopotea…… Mungu, ambaye hana kikomo katika Roho, kuikomboa jamii iliyopotea ya binadamu, Mungu Mwenyewe alifanyika jamaa aliye karibu, Mtu, Mwana aliyemuumba katika tumbo la uzazi la Mariamu.(Yohana1:1-18; Wafilipi 2:5-11). Halafu Yeye akafanya ishara, ama ushuhuda; nje ya milango ya Yerusalemu. Yeye aliinuliwa kati ya mbingu na nchi, kisha akafa, na kukomboa kila kitu. Na katika kutokwa na damu, Yeye alilitakasa Kanisa ili kwamba Yeye Mwenyewe apate kuishi mle ndani, na kufanya ushirika na kushiriki nalo, ile sehemu iliyopotea ya ushirika tangu bustani ya Edeni ambamo Mungu alishuka kila jioni, wakati wa kanisa.Uliona, Mungu alishuka akaja wakati wa jua kupunga, machweo ya jua. Kuna kitu fulani kuhusu wakati inapoanza kuwa giza, watu wanafikiri juu ya kanisa pamoja na Mungu; Wakristo. Unaona jua likitua, unatambua kua jua lako linatua.

Basi katika wakati wa jua kupunga Yeye angeshuka na kushiriki pamoja nao. Ndipo hapo akapoteza ule ushirika, kwa maana dhambi isingemruhusu kufanya jambo hilo.Halafu basi alifanyika mwili akakaa kwetu, kusudi apate kurudi tena kwa mwanadamu, na kuishi katika mwanadamu, na kumrudisha mwanadamu katika hali ya ushirika pamoja Naye tena, na kumrudishia haki zake alizopewa na Mungu. Hivyo ndivyo alivyofanya.

Hilo ndilo kusudi la Roho Mtakatifu. Ni Baba, tena, Mungu Baba akiishi ndani yako, akitekeleza mipango Yake, kumaliza mpango Wake wa ukombozi; akifanya kazi kupitia kwako, akikufanya mfanya kazi pamoja Naye; akikupa mahali fulani, akikupa sehemu fulani kwa ajili ya ndugu na dada yako walioanguka; akikupa wewe Roho Wake na upendo Wake, wa kwenda kuwatafuta waliopotea, kama alivyofanya katika bustani ya Edeni. “Adamu, Adamu, uko wapi?” Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu anavyomfanyia mwanamume ama mwanamke. Hapo Yeye anapougusa moyo wao na kupata kikao Chake, kuna kiu na kuona njaa kwa ajili ya watu waliopotea.(Mithali 11:30; Mithali 24:11-12). Hiyo ndiyo shida ya mikutano siku hizi. Hamna mguso wa kutosha wa Roho mle, kuenda kawatafuta waliopotea na wanaokufa. Zaidi sana ni kwa ajili ya kujifanyia jina, ama kanisa, ama jengo, ama madhehebu, badala ya mpango wa kuwavuta watu. Ni jambo la kusikitisha jinsi gani.

Mungu alijimwaga Mwenyewe katika Kristo. Kweli. Kristo alijimwaga katika Kanisa.(Wakolosai 2:9-10)“Siku ile mtatambua ya kwamba Mimi ni ndani ya Baba Yangu, nanyi mko ndani Yangu, Nami niko ndani yenu. (Yohana 14:18-20)Siku ile mtajua jambo hilo.” Kwa kuwa, jambo lote ni mpango mmoja wa ukombozi ukishuka, kwamba Mungu anarudi kuishi ndani, na kuishi pamoja, na kushiriki pamoja na watu Wake, kama alivyofanya hapo mwanzo.Sasa, basi, mara anapolifanya Kanisa Lake kuwa katika hali ya kuzungumza, anapoliweka Kanisa Lake mahali ambapo anaweza kujiingiza ndani, na kupenda, na kushawishi, na kushiriki, basi Edeni itatokea. Atalirudisha Kanisa Lake mahali ambapo li—lilipomwacha Yeye, kurudi kwenye Edeni tena, mahali pale lilipoangukia. Hilo, sasa… Hapo ndipo lilipoanza mara ya kwanza, ama lilipoangukia. Hapo ndipo litakaporudishwa moja kwa moja, pamoja na kila hali ya usafi ya ukombozi, kuwarudisha moja kwa moja mahali hapo tena. [17]

Angalia,Mungu alikua na Makusudio matatu katika hii siri kuu mno. Mungu, Katika siri yake kuu sana ambayo alikua nayo kabla ya kuanza kwa ulimwengu, Yeye alikua na makusudio matatu ndani yake.Makusudio hayo matatu ni yapi? Sasa, naamini kwa msaada wa Mungu, ambaye yuko hapa, na yeye atatuonyesha hilo sisi. Sasa,Kama yeye alikua na makusudio haya matatu, Tunataka kujua haya makusudio matatu ni yapi.

Jambo la kwanza lilikua kwamba Mungu alitaka kujufunua mwenyewe kwa watu.Lakini yeye alitaka kufanya nini, Yeye alipenda kua Baba, kwamaana yeye alikua Baba.Na njia pekee ambayo yeye angeweza kujieleleza hilo ni kwa kua Mwana wa adamu.Hiyo ndio sababu Yesu alikua akisema, “Mwana wa adamu” (Mathayo 8:20; 9:6; 12:8,32,40). Unaona, hawakujua kile yeye anazungumzia kulihusu, wengi wao. Lakini sasa mnalipata hilo? Yeye alitaka kujieleleza mwenyewe.Hilo lilikua miongoni mwa makusudio yake makuu matatu, ilikua kujieleleza mwenyewe, Kujitambulisha mwenyewe na wanadamu, kujidhihirisha mwenyewe ndani ya Kristo (II Wakorintho 5:19; Wakolosai 2:9-10).

Pili: Kua na utangulizi katika mwili wake wa waamini,hivyo ndivyo, Bibi harusi wake, kwamba angeweza kuishi ndani ya watu.

Wakati ninapoona makusudio ya Mungu makuu: Kwanza kujidhihirisha mwenyewe ndani ya kristo, Ukamilifu wa mwili wa Kichwa cha Mungu, halafu tena kuleta ule Ukamilifu wa mwili wa kichwa cha Mungu ndani ya watu ambao angeweza kupata utangulizi, uangalizi, uongozi.

Na la tatu, kurejeza Ufalme katika hali yake ambao ulianguka kwasababu ya kwa Adamu wa kwanza,kurudi pale ambapo alitembea katika jioni tulivu Na watu wake, akizungumza nao, akifanya ushirika nao. [20]

*‘’…..ili lisimame kusudi la Mungula kuchagua ……..”* (Warumi9:9-11)

Kama tumewekwa hapa kwa makusudi, basi hakuna litakalo tudhuru sisi mpaka mpango wa Mungu umetimizwa.Hakuna kitakacho tudhuru mpaka ule mpango ambao Mungu ametuweka sisi hapa kwaajili yake uwe umedhihirishwa. Mpango wa Mungu kamwe hauwezi kushindwa. Hakuna kitakachoushinda huo. Hivyo tunapaswa kua watu wafuraha namna gani leo, kupumzika juu ya ufunuo wa Neno la Mungu aliye hai, kwamba hakuna jambo sasa ama jambo ambalo lingeweza kuja; hakuna magonjwa, hakuna huzuni, hakuna kifo, hakuna hatari, ama chochote kinachoweza kututenga sisi na mpango wa Mungu aliye hai (warumi 8:35-39)

Nabii amezungumza juu ya uzoefu alionao:

Na nilikua nimechoka sana, ikionekana kama moyo wangu ungewezakuacha kudunda. Na wakati nilipokua nikiketi pale, kwa haraka yote ningeweza kusikia kila mmoja akisema, lakini ilionekana kama nilikua nje ya dunia.Nikawaza, ''Je nina shambulio la moyo?'' Na nikaondoka kwenye kiti chake cha kinyozi. Nikawaza, ''si ajabu kama hilo ndilo lililotokea?'' Nikashusha mikono yangu. Wanahesabika,na moyo wangu ulionekana kama ulikua ukiacha kupiga. Na nikawaza ''loo! Lakini kuna….. Injili inayotakiwa kuhubiriwa. Na hakuna nguvu inayoweza kuunichukua mimi mpaka mpango wa mungu umetimizwa" Hakuna kinachoweza kunidhuru,hakuna jambo, mpaka mpango wa Mungu uwe umetimizwa. Na wakati hilo linapotimia, Nataka kwenda na mpango wake.

Wakati yeye anapomaliza, basi na mimi nimemaliza pia.Wakati anapomaliza na mimi, mimi ninakua nimemaliza na haya maisha.Wakati anapomaliza na wewe, wewe umemaliza pia.Kwahiyo inaleta tofauti gani?Mungu anashikilia yote mkononi mwake.

Haijalishi sisi tuvijana ama wazee,hatujui ni lini kusudio la Mungu litakapotimizwa na kumalizika.Mungu huchukua watoto wadogo wakati mwingine kuonyesha kwamba anaweza kuongoza nafsi zao ndogo.Kila kitu afanyacho ni kwa kusudio (warumi8:28-30). Yeye alisema, hakuna hata mbayuwayu angeweza kudondoka kutoka mbinguni bila ya yeye kujua hilo.Kila kitu huenda kwa kusudi lake kwa wakati wake na majira yake.Yako yote katika mpango wake wa kiungu.Hakuna kitakacho haribu.

Inaenda kutonyesha tu kua hakuna kinachoweza kushinda kusudio lake.Hata kifo hakiwezi kulishinda kusudio lake.Ibrahimu alikua kama tu mfu, na tumbo la sara lilikua limekufa kwa miaka arobaini ama hamsini.Lakini hakuna kitakachoshinda kusudio la Mungu (warumi 4:16-22) Mwili wake ulikua umezeeka,umechoka(kasoro).Mishipa ya maziwa ilikua imekauka kabisa.Moyo wake ulikua dhaifu sana, haungeweza kwenda leba.Lakini Mungu alituacha tujua pale kua kusudio lake haliwezi kushindwa.

Basi haijalishi magonjwa yatakuja jinsi gani,aina gani ya kifo tunakufa,umaskini wa namna gani tunapitia, Kusudio la Mungu haliwezi kushindwa.Yeye atatufufua sisi tena."Kwasababu ninaishi,nanyi mtaishi pia" (yohana 14:19). Hilo ndio tumaini letu. [21]

<u>Nukuu:</u>

[1]"Makao ya baadae"(64-0802),aya 237-238,242
[2]'Dhihaka kwasababu ya Neno'(62-1223)aya 81
[3]'Shalom'(64-0112) aya 230/182

[4]Mungu akijificha mwenyewe katika urahisi (63-0317M) aya 391-392

[5]"Karama za Mungu daima hupata mahalipao" (63-1222), aya 77

[6]”Ufunuo sura ya 4 sehemu 3” (61-0108), aya 255

[7]”Milango ndani ya mlango” (65-0206), aya 86-88

[8]”Kuchulua upande pamoja na Yesu” (62-0601), aya 98

[9]”Kufanywa wana wenyewe mamlaka,sehemu ya IV”(60-0522E), aya 212

[10]”Sikukuu ya baragumu” (64-0719M), aya 186-187

[11]”Yakini” (62-1230M), aya 332-336

[12]”Uhakika wa Mungu aliyehai usioshindwa” (60-0626), aya 241/ aya 73,82

[13]”Kumkumbuka Bwana”(62-1209) aya 35-39

[14]’Kuhesabu kinyumenyume” (64-0209) aya 28

[15]”Mimi ni Ufufuo na Uzima”(63-1118), aya 37

[16]”Umoja wa Mungu mmoja katika kanisa moja”(58-1221E) aya 33

[17]”Roho Mtakatifu alitolewa kwa kusudi gani”(59-1217) aya 19/ 23-24/ 29-32

[18]”Maswali na Majibu juu ya Roho Mtakatifu”(59-1219) aya 45

[19]”Ushirika kupitia upatanisho’(55-0605) aya E15

[20]”Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa”(63-0728) aya 140-144, 146, 156

[21]’Ninajua mteteziwangu anaishi” (58-0406S) aya E12-13, E22-29